THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/2 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasioko Shuleni)

MUDA: Saa 2:30 ***Ijumaa, 09 Oktoba 2009 mchana***

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4)**, swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Mashine za hesabu za elektoniki **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi.

Scanned by CamScanner

BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIIM

SEHEMU A: QUR'AN

1. Andika tafsiri ya suratu-Alam-Nashrah kisha eleza ujumbe wa sura hiyo.

2. *Hakika Sisi tumeiteremsha Qur'an kwa Kiarabu ili mupate kufahamu.(12:2)* Oanisha ujumbe wa aya hii na mpango wa Allah (s.w) kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) ni kwa ajili ya walimwengu wote.

3. Eleza hoja tano (5) zilizomo ndani ya Qur'an kuthibitisha kuwa Qur'an ni Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu

SEHEMU B: TAWHIID

4. Eleza maana ya kumuamini Mtume Muhammad (s.a.w) katika mchakato wa maisha ya kila siku ya Muislamu ?

5. *Soma, na Mola wako ni Karimu sana. Ambaye amemfundisha (binaadamu elimu zote hizi) kwa wasita (msaada) wa kalamu ; Amemfundisha mwanadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui. (96:3-5)*
Kwa kutoa mifano hai, bainisha mbinu tano (5) alizotumia Mwenyezi Mungu kuwasiliana na waja wake.

6. Toa maelezo mafupi juu ya aina kuu mbili za dini, kisha onyesha ni kwa nini mwanadamu hawezi kuishi bila dini.

SEHEMU C: FIQH

7. Eleza jinsi Sunnah zinazoambatana na swaumu ya mwezi wa Ramadhani zinavyomsaidia mfungaji kufikia lengo la funga.

8. Toa maelezo mafupi juu ya aina za talaka zifuatazo:
   (a) Talaka rejea
   (b) Talaka tatu
   (c) Talaka ya 'ilaa
   (d) Talaka ya khul
   (e) Talala ya zihaar

9. Toa hoja nne (4) kuonesha hekima ya Mwenyezi Mungu kutoa ruhusa ya kuoa wake hadi wanne.

toto print uk.

Scanned by CamScanner

SEHEMU D: TAREKH

10. Ni kwanini Bani israil walighadhibikiwa na Mwenyezi Mungu?

11. Eleza chokochoko tano (5) za Mayahudi dhidi ya Dola ya Kiislamu Madinah.

12. *Wanataka kuzima Nuru ya Mwenyezi Mungu (ya Uislamu) kwa vinywa vyao; na Mwenyezi Mungu atakamilisha Nuru Yake ijapokuwa makafiri watachukia (61 :8).*
Chambua mbinu tano (5) walizotumia makafiri kutaka kuzima nuru ya Uislamu katika kipindi cha Mtume akiwa Makka.

Scanned by CamScanner